MAELEZO MAFUPI YA MKURUGENZI WA MAENDELEO YA VIJANA. BW. JAMES KAJUGUSI WAKATI WA KUFUNGUA SEMINA YA VIJANA WA VYUO VYA ELIMU YA JUU KUHUSU WAJIBU WA VIJANA KATIKA KUIMARISHA MUUNGANO MIAKA 50 BAADA YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR UKUMBI WA UBUNGO PLAZA JUMAPILI MACHI 30, 2014

Ndugu Wawezeshaji wa Semina hii Prof Issa Shivji na Prof. Gaudens Mpangala,

Ndugu Vijana, Wanafunzi kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu,
Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,
Habari za Asubuhi,

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha katika Kongamano la Vijana wa Vyuo vya Elimu ya Juu kuhusu Wajibu wa Vijana katika Kuimarisha Muungano Wetu, Miaka 50 baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar inayofanyika hapa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Namshukuru Mungu kwa kutuwezesha wote kufika hapa salama ili tuweze kushiriki katika Kongamano hili muhimu hasa katika kipindi hiki tunaposherehekea miaka 50 ya Muungano wetu.

Naomba nianze kwa kuwashukuru Wahadhiri wetu Waandamizi Profesa Gaudens Mpangala na Profesa Issa Shivji kwa kukubali kuja kutoa mhadhara katika Kongamano hili muhimu katika kuimarisha Muungano wetu . Pamoja na majukumu yao mengi wameona ni vyema wakaja kushiriki nasi katika siku ya leo. Nakushukuru sana.

Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Mtakubaliana na mimi kwamba kundi la Vijana linachukua nafasi kubwa katika nguvu kazi ya taifa letu hivyo kuna haja ya kukumbushwa historia ya nchi yetu ambayo imekuwa chachu ya Muungano, Mshikamano, Umoja, Upendo na Amani iliyodumu kwa zaidi ya miaka 50 tangu nchi zetu zipate Uhuru na kuungana kuwa nchi moja yenye Serikali mbili mwaka 1964.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unafikisha miaka 50 tangu kuasisiwa kwake April 26, 1964 na waasisi wa Taifa letu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mzee wetu Abeid Aman Karume, Rais wa Kwanza wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Kutokana na umuhimu wa sherehe za miaka 50 za kuadhimisha Muungano wetu, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo yenye jukumu la kusimamia sekta ya Vijana imeandaa Kongamano la Vijana kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu kuhusu Wajibu wa Vijana katika Kuimarisha Muungano Wetu Miaka 50 tangu kuzaliwa kwake.

Kauli mbiu ya sherehe za Miaka 50 ya Muungano ni "**UTANZANIA WETU NI MUUNGANO WETU, TUULINDE, TUUIMARISHE NA KUUDUMISHA".**

Lengo la Kongamano hili ni kuzungumzia Wajibu wa Vijana katika kuimarisha Muungano ambao mwezi ujao unafikisha miaka 50.

Bila shaka wengi wa Vijana tuliokutana hapa wakati Muungano huu unaasisiwa hamkuwepo na pamoja na kwamba hamkuwepo ndio mnaoshikilia dhamana ya Taifa hili kutokana na uwingi wenu pamoja na mategemeo ya jamii yetu kwenu.

Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Washiriki wa Kongamano hili ni vijana 300 kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyopo Tanzania Bara na Zanzibar. Washiriki 270 wanatoka katika Vyuo vifuatavyo :- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ualimu (DUCE), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Chuo cha Biashara (CBE), Chuo cha Ustawi wa Jamii, Chuo Kikuu cha St John's, Chuo cha Ufundi na Teknolojia (DIT), Chuo cha Diplomasia, Kampala University, Chuo cha Uhasibu (TIA), Chuo Kikuu cha Sayansi na Afya ya Jamii Muhimbili , Chuo cha Usafirishaji (NIT), Chuo Kikuu Huria, Chuo cha Azania, Chuo cha Ununuzi na Ugavi (IPS), Chuo cha Bandari, Chuo cha Maji, na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Kivukoni.

Washiriki wengine 30 kutoka Zanzibar ni pamoja na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar, Chuo cha Usimamizi wa Fedha na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Washiriki wa Kongamano hili watapata fursa ya kuwasikia watoa mada ambao ni Wahadhiri wa Chuo Kikuu Prof. Gaudens Mpangala atakayewasilisha mada kuhusu Wajibu wa Vijana katika Kuimarisha Muungano, Miaka 50 tangu kuzaliwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Aidha mada kuhusu Mapendekezo ya Katiba Mpya kwa Mustakabali wa Muungano wetu itawasilishwa na Prof. Issa Shivji.

Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Wizara yetu ina jukumu la kusimamia sekta Nne muhimu ikiwemo sekta ya Maendeleo ya Vijana. Kutokana na umuhimu wa Kongamano hili tungependa kuwaalika Vijana wote kushiriki lakini kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu tumewaalika washiriki 300 kwa niaba ya wenzao kushiriki katika kongamano hili leo hii.

Aidha, kupitia vyombo vya Habari ni matumaini yangu vijana wengi watapata nafasi ya kufahamu yale yote yanayoendelea katika Kongamano hili. Tumealika Vyombo vya Habari vikiwemo Magazeti, Radio, Televisheni na wanaoendesha Mitandao ya Kijamii ili waweze kushiriki nasi na kuweza kutoa taarifa kwa umma. Aidha, Televisheni ya Taifa (TBC One) na TBC Taifa vimealikwa kutoa matangazo ya moja kwa moja.

Napenda nivishukuru Vyombo vya Habari nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuelimisha na kuuhabarisha umma kuhusu mafanikio tuliyoyapata ndani ya miaka 50 wa muungano wetu. Taarifa zao zimekuwa zinasaidia kuimarisha, kuudumisha na kuulinda muungano wetu.

Ndugu Washiriki, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Baada ya kusema haya machache naomba sasa niwakaribishe rasmi tuanze ratiba yetu kwa Prof. Gaudens Mpangala kuwasilisha mada yake kuhusu Wajibu wa Vijana katika kuimarisha Muungano wetu..

Karibu!!!!!!!!!!